# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1010

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Falsafa na Maadili ya Ualimu Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-747-0

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Falsafa na Maadili ya Ualimu Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA FALSAFA NA MAADILI YA UALIMU STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA AWALI

## 2023

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2023
Toleo la Kwanza, 2023

ISBN: 978-9987-09-747-0

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Somo la Falsafa na Maadili ya Ualimu Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

**Yaliyomo**

Orodha ya majedwali .................... iv
Vifupisho .................... v
Shukurani .................... vi

1.0 Utangulizi .................... 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania .................... 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu .................... 2
    3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu .................... 2
    3.2 Malengo mahususi ya Elimu ya Ualimu .................... 2
4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu .................... 2
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi .................... 3
6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ujifunzaji na Ufundishaji .................... 4
    6.1 Mkufunzi .................... 4
    6.2 Mwalimu Tarajali .................... 4
    6.3 Mzazi/Mlezi .................... 4
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji .................... 5
8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji .................... 5
9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji .................... 5
10.0 Idadi ya Vipindi .................... 7
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji .................... 7

Bibliografia .................... 10

## Orodha ya majedwali

Jedwali Na 1: Umahiri mkuu na umahiri mahususi (Mwaka wa kwanza) ....................3

Jedwali Na 2: Alama za upimaji endelevu kwa masomo ya utaalamu na ya jumla.................... 7

Jedwali Na 3: Maudhui ya Mwaka wa kwanza .................... 8

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |

## Shukurani

Maandalizi ya muhtasari wa Somo la Falsafa na Maadili ya Ualimu yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala wa TET. Vilevile, Taasisi inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndio lengo kuu la uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Somo la Falsafa na Maadili ya Ualimu ni la lazima katika mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali. Ujifunzaji wa somo hili utamwezesha mwalimu tarajali kuwa na uwezo wa kuchambua falsafa na misingi mbali mbali ya elimu pamoja na miongozo inayosimamia maadili, wajibu na haki ya mwalimu. Somo hili litamwezesha mwalimu tarajali kukuza uwezo wa kuwa na misimamo ya kimaadili kwa njia huru zaidi. Hivyo, mwalimu tarajali anapaswa kua mfano mzuri wa kuigwa na kumsaidia mwanafunzi kua mwaminifu, mdadisi, mzalendo na mwenye kujiamini katika mambo mbalimbali yanayohusu maadili ya kitanzania.

Aidha, Muhtasari huu umeandaliwa kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Falsafa na Maadili ya Ualimu ngazi ya Stashahada ya Elimu ya Awali kwa kuzingatia Mtaala wa Stashahada ya Ualimu Tanzania Bara wa mwaka 2023. Muhtasri unatoa maelekezo ya kumwezesha mkufunzi kuandaa mchakato wa ufundishaji kwa ufanisi. Vilevile, muhtasari unatoa nafasi kwa mkufunzi kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Falsafa na Maadili ikiwemo namna ya kuchopeka masuala mtambuka na kutumia TEHAMA.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku; na

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu

### 3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu

Kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 3.2 Malengo mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo ya Elimu ya Ualimu ni kumwezesha mwalimu tarajali:

(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha na misingi ya ualimu;

(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;

(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;

(e) Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;

(f) Kukuza stadi za utambuzi wa awali kwa mwanafunzi mwenye mahitaji ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;

(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji; na

(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani, *classroom-based research*).

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu

Umahiri wa jumla utakaojengwa na Mwalimu tarajali ni:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;

(d) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi;

(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ujifunzaji na ufundishaji;

(f) Kumtambua mwanafunzi mwenye mahitaji ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;

(g) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;

(h) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (yaani, *instructional leadership*); na

(i) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani, *classroom-based research)*.

**5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi**

Jedwali lifuatalo linaonesha umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa na mwalimu tarajali.

**Jedwali Na 1:** *Umahiri mkuu na umahiri mahususi (Mwaka wa kwanza)*

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu falsafa na maadaili ya Ualimu | 1.1 Kuchambua falsafa na misingi ya elimu.<br>1.2 Kutathmini maendeleo ya elimu ya awali duniani.<br>1.3 Kutambua maadili, wajibu na haki ya mwalimu. |

**6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji**

Ufundishaji na ujifunzaji katika somo la Falsafa na Maadili Ualimu Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Awali unategemea ushirikiano baina ya mkufunzi, mwalimu tarajali na mzazi/mlezi katika kutimiza wajibu wao ambao ni:

### 6.1 Mkufunzi

Mkufunzi anatarajiwa:

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Baadhi ya mbinu zinazopendekezwa ni zile zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana;

(c) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao; na

(d) Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahiki;

### 6.2 Mwalimu Tarajali

Mwalimu Tarajali anatarajiwa:

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri stahiki katika maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ufundishaji na ujifunzaji, mbinu za kufundishia na kujifunzia na mbinu za upimaji zitakazomwezesha kubaini mafanikio na kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo. Baadhi ya nadharia hizo ni haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia, kuandaa na kutumia vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kutathmini mwanafunzi;

(c) Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu;

(d) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na

(e) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

### 6.3 Mzazi/Mlezi

Mzazi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji; na

(b) Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika ujifunzaji.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji Somo la Falsafa na Maadili ya ualimu Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali utafanyika kwa vitendo zaidi ili kumwezesha mwalimu tarajali kushiriki kikamilifu katika vitendo vya ujifunzaji na kukuza stadi za karne ya 21. Mkufunzi anashauriwa kutumia mbinu shirikishi na stahiki zitakazomwezesha mwalimu tarajali kujenga umahiri uliokusudiwa. Mbinu zinazopendekezwa kutumika ni pamoja na michezo, nyimbo, maigizo, uchunguzi, ngonjera, kazimradi, majadiliano, matembezi ya galari, kumualika mgeni, igizo dhima na hadithi. Mkufunzi anashauriwa kuwa mnyumbufu na kutumia mbinu nyingine zinazoendana na mazingira husika ambayo ni rafiki na shirikishi kwa walimu tarajali.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Ualimu Elimu ya Awali zinapaswa kuwa shirikishi na zinazokidhi mahitaji ya ujifunzaji. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha kuwa mwalimu tarajali anapata nafasi ya kuona, kusikia, kushika na kujifunza uandaaji na utumiaji wa zana au vifaa mbalimbali vya ujifunzaji na ufundishaji. Aidha, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa kumsaidia mwalimu tarajali kuelewa anachofundishwa. Mkufunzi anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira au kufaragua zana ambazo zitamsaidia Mwalimu tarajali kujenga tabia ya udadisi, ugunduzi, kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, kukuza fikra tunduizi, utatuzi wa matatizo, ujuzi wa kidijitali na uzalendo. Zana hizo zimependekezwa katika jedwali Na.3 la maudhui katika kipengele cha zana/vifaa.

## 9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji

Upimaji ni mchakato muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji ili kufikia malengo ya elimu yaliyokusudiwa. Upimaji wa somo la

Falsafa na Maadili ya Ualimu utazingatia upimaji endelevu na tamati ili kutambua uwezo na mahitaji ya ujifunzaji ya mwalimu tarajali. Upimaji huu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji ili kufikia ujenzi wa umahiri wa mwalimu tarajali uliokusudiwa. Mbinu za upimaji wa maendeleo kama mitihani, majaribio, mazoezi, hojaji, bungua bongo, maswali ya papo kwa papo, mkoba wa kazi na kazimradi zinategemewa kutumika ili kupima ujifunzaji wa mwalimu tarajali. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha anampima mwalimu tarajali katika nyanja zote za upimaji ambazo ni maarifa, stadi na mwelekeo. Aidha, ni muhimu kufanya tathmini ya maendeleo ya mwalimu tarajali ili kubaini kiwango cha utendaji alichofikia katika nyanja zote za ujifunzaji. Matokeo ya tathmini yatasaidia kufanya uboreshaji ili kuhakikisha malengo ya Elimu ya Ualimu Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali yamefikiwa.

Mkufunzi anapaswa kubuni shughuli nyingi zaidi za upimaji ili kuchochea ujifunzaji. Upimaji wa mwisho utachangia asilimia sabini (70%) na upimaji endelevu utachangia asilimia thelathini (30%). Aidha, mwalimu tarajali anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia hamsini 50% na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafaulu, mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu.

**Jedwali Na 2:** *Alama za upimaji endelevu kwa masomo ya utaalamu na ya jumla*

| **Na.** | **Shughuli ya Upimaji** | **%** |
|---|---|---|
| 1. | Mtihani wa Muhula wa I kwa Mwaka wa I | 6.0 |
| 2. | Mtihani wa Muhula wa II kwa Mwaka wa I | 6.0 |
| 3. | Mtihani wa Muhula wa I kwa Mwaka wa II | 6.0 |
| 4. | Kazi Mradi (Project) | 7.0 |
| 5. | Mkoba wa Kazi | 5.0 |
| **Jumla** | | **30** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo la Falsafa na Maadili ya Ualimu Elimu ya Awali unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za ujifunzaji. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika sitini (60). Somo hili lina idadi ya vipindi viwili (2) kwa wiki.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji yamepangiliwa katika vipengele sita ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, vigezo vya upimaji, zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia na idadi ya vipindi. Jedwali Na 3 linaonesha maudhui yanayopaswa kufundishwa katika ngazi ya Elimu ya Ualimu wa Elimu ya Awali.

**Jedwali Na 3:** *Maudhui ya Mwaka wa Kwanza*

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu falsafa na maadili ya Ualimu | 1.1 Kuchambua falsafa na misingi ya elimu | (a) Kufafanua dhana ya falsafa ya Elimu ya Awali (*maana, uhusiano kati ya elimu na falsafa* na *umuhimu wa Falsafa ya Elimu*) | Dhana ya falsafa ya elimu imefafanuliwa kwa kuzingatia maana, uhusiano kati ya elimu na falsafa na umuhimu wa Falsafa ya Elimu | Matini na machapisho mbalimbali yanayoeleza dhana na chimbuko la Elimu ya Awali | 39 |
| | | (b) Kuchambua dhana ya Elimu ya Awali (*maana* na *chimbuko*) | Dhana ya Elimu ya Awali imechambuliwa kwa kuzingatia maana na chimbuko | | |
| | | (c) Kuchambua misingi ya kifalsafa ya Elimu ya Awali (*mf. Maria Montessori, Jean-Jacques Rousseau, Johann Pestalozzi, Friedrich Froebel* na *John Dewey*) | Misingi ya kifalsafa ya Elimu ya Awali imechambuliwa kwa kuzingatia falsafa ya *Maria Montessori, Jean-Jacques Rousseau, Johann Pestalozzi, Friedrich Froebel* na *John Dewey*. | | |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kutathmini maendeleo ya Elimu ya Awali duniani | (a) Kuchambua maendeleo ya Elimu ya Awali kimataifa na kitaifa | Maendeleo ya Elimu ya Awali kimataifa na kitaifa yamechambuliwa | Matini na machapisho yanayoeleza matamko, vihunzi na sera za kimataifa na kitaifa kuhusu maendeleo ya Elimu ya Awali | 12 |
| | 1.3 Kutambua maadili, wajibu na haki ya mwalimu | (b) Kuchambua dhana ya maadili, wajibu na haki ya mwalimu | Dhana ya maadili, wajibu na haki ya mwalimu zimechambuliwa | Matini zinazoeleza dhana ya maadili, wajibu na haki ya mwalimu, picha mnato, video, chati yenye picha zinazoonesha mavazi yanayostahili na yasiyostahili kwa mtumishi wa umma | 21 |
| | | (c) Kuchambua miongozo inayosimamia maadili, wajibu na haki ya mwalimu | Miongozo inayasimamia maadili, wajibu na haki ya mwalimu imechambuliwa | Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kanuni za maadili ya utumishi wa Umma, ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu, sheria na kanuni za Tume ya utumishi wa walimu, mwongozo wa utumishi wa Umma (Standing Orders for public service in Tanzania) na skimu ya Utumishi wa walimu | |

**Bibliografia**


Bholah, R., Nenduradu, R., & Thaunoo, J. (2022). Preparing Early Years Practitioners in Mauritius. In Play and STEM Education in the Early Years: International Policies and Practices (pp. 251-272). Springer International Publishing.

Campbell, E. (2003). *The Ethical Teacher*. Open University Press

Carr, D. (2000). Education, profession and culture: Some conceptual questions. *British Journal of Educational Studies, 48*(3), 248 – 268.

Carr, D. (2000). *Professionalism and ethics in teaching*. Routledge.

Carr, D. (2003). Moral educational implications of rival conceptions of education and the role of the teacher. *Journal of Moral Education, 32*(3), 219-232.

Clough, P., & Nutbrown, C. (2014). Early childhood education: History, philosophy and experience. *Early Childhood Education*, 1-216.

Dahlberg, G., Moss, P., & Pence, A. R. (1999). *Beyond quality in early childhood education and care: Postmodern perspectives*. Psychology Press.

Essa, E. L., & Burnham, M. M. (2019). *Introduction to early childhood education*. Sage Publications.

Farquhar, S., & White, E. J. (2014). Philosophy and pedagogy of early childhood. *Educational philosophy and theory, 46*(8), 821-832.

Gensler, H. J. (2017). *Ethics: A contemporary introduction*. Routledge.

Gianoutsos, J. (2006). Locke and Rousseau: Early childhood education. *The Pulse, 4*(1), 1-23.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania [JMT]. (1995). *Sera ya Elimu na Mafunzo*. Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania [JMT]. (2014). *Sera ya Elimu na Mafunzo*. Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Krogh, S. L., & Slentz, K. L. (2010). *Early childhood education: Yesterday, today, and tomorrow*. Routledge.

Ministry of Education and Culture. (2004). *National curriculum guidelines on early childhood education and care in Finland*. Finish national agency for education.

Ministry of Education, Culture and Human Resources. (2009). *National curriculum framework pre-primary*. Mauritius institute of education & early childhood care & education.

Ndibalema, P. (2013). *Professionalism and ethics in education: A handbook for prospective teachers*. Creative Prints.

Nyirenda, S.D & Ishumi, A.G. M (Eds). (2002). *Philosophy of education: An introduction to concepts, principles and practice*. Dar es Salaam University Press.

Pring, R. (2001). Education as a moral practice. *Journal of Moral Education, 30*(2), 101-112.

Republic of Namibia. (2015). *Pre-primary syllabus english version*. Ministry of Education.

Republic of South Africa. (2015). *The south African national curriculum framework for children from birth to four.* Department of basic education.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. (2022). *Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: chimbuko, misingi na maendeleo*: Dar es Salaam.

Tassoni, P. & Hucker, K. (2000). *Planning play and the early years*. Heinemann Educational Publishers.

Tume ya Utumishi wa Walimu [TSC]. (2013). Ufafanuzi wa Kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu. Imepakuliwa kutok http://www.tsc.go.tz

United Republic of Tanzania [URT]. (1996). The Code of Ethics and Conduct for the Public Service Tanzania. Imepakuliwa kutoka http://www.tsc.go.tz

URT. (2016). The Local Government Scheme 2016. Imepakuliwa kutoka http://www.tsc.go.tz

Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekinolojia. (2016). *Mtaala na muhtasari wa elimu ya awali*. Taasisi ya Elimu Tanzania.